

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**



TAARIFA KWA UMMA

DKT. NCHEMBA AWAKARIBISHA WAWEKEZAJI KUTOKA MISRI

Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba amewakaribisha Wawekezaji kutoka Jamhuri ya Kiarabu ya Misri kuwekeza na kufanya biashara na Tanzania kutokana na uwepo wa mazingira rafiki na fursa za uwekezaji.

Waziri Nchemba ametoa rai hiyo mjini Cairo Misri, wakati wa Kongamano la Kimataifa la Ushirikiano la Misri (*Egypt International Cooperation Forum*) lililowakutanisha wadau mbalimbali wakiwemo washirika wa maendeleo kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Ulaya, Jumuiya ya Ushirikiano wa Uchumi na Maendeleo, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia.

Dkt. Nchemba alisema kuwa kuna umuhimu wa kusisitiza kukuza mahusiano ya kimataifa hususan kwa nchi za kiafrika zinazoendelea na kuweka mikakati endelevu ya kupambana na athari za janga la Uviko - 19, ili kukuza uchumi.

“Katika Kongamano hili tumejadilia namna bora ya kusaidiana katika mitaji hususan katika nchi zenye Taasisi za Kifedha zenye uwezo wakutoa fedha katika mazingira ya Uviko- 19 kutokana kuathiri shughuli nyingi za kiuchumi”, alieleza Dkt. Nchemba.

Aidha Dkt. Nchemba ameipongeza Wizara ya Ushirikiano ya Kimataifa ya Jamhuri ya Kiarabu ya Misri kwa kuandaa kongamano hilo kwa kuwa limeunganisha wadau kutoka sehemu mbalimbali duniani na kutoa fursa ya kuweza kujadiliana na kupeana uzoefu kwa lengo la kuleta maendeleo.

Vilevile ameahidi kuwa Serikali ya Tanzania itaendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Kiarabu ya Misri katika nyanja mbalimbali ikiwemo masuala ya uchumi, uwekezaji na biashara ili kukuza uchumi kati ya nchi hizo.

Kongamano la Kimataifa la Ushirikiano la Misri (*Egypt International Cooperation Forum*) linalofanyika kwa siku 2 limehudhuriwa na nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania, Malawi, Senegal, Kenya, Namibia na Zambia.

Imetolewa na:

**Benny Mwaipaja
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Fedha ya Mipango**